

I am GIRLRISING 10



Ili kuadhimisha muongo mmoja wa Girl Rising, tunakualika kushiriki katika kamjeni ya “I Am Girl Rising 10.” Kamjeni hii inasisitiza kuhusu maono na vitendo vya watu kote duniani ambao ni watetezi wa mabadiliko ya kujenga haki bora zaidi za baadaye. Kushiriki kwako katika kamjeni hii ni muhimu-Tunataka kusikia sauti yako kwa kushiriki. Kushiriki ni rahisi! Unachostahili kufanya ni kutumia simu yako kujirekodi ukishiriki katika ujumbe wa “I am Girl Rising” ukiwa na ujumbe wa Girl Rising ulioandikwa kwenye mkono wako. Kisha utume video yako kufikia Septemba tarehe 3. Tumeweka maelezo hapa chini na pia mifano ya video na ujumbe.

Jinsi ya kupiga filamu ya video yako.

Ili kuhakikisha kuwa video yako ni ya hali ya juu na yenye athari nzuri fuata maelekezo haya:

1. Weka simu yako wima ili kurekodi video zako.
2. Hakikisha sehemu uliyoko ina mwangaza wa kutosha. Mwangaza wa asili ni bora zaidi kwa hivyo jielekeze kwenye dirisha au uwe nje mahali penye kivuli. Hakikisha mwangaza uko mbele yako k.m hakuna dirisha lenye mwangaza zaidi au taa nyuma yako.
3. Hakikisha sauti inasikika vizuri. Rekodi video katika sehemu tulivu. Zungumza vyema na kwa mwendo taratibu. Unaweza kutumia spika za masikio kama zina maikrofoni nzuri.
4. Mavazi na usuli. Rangi imara kwa mavazi ni bora zaidi. Piga filamu katika katika usuli usio na mchanganyiko.
5. Kuwasiliana kwa macho ni muhimu. Hakikisha kuwa unaangalia kamera kila wakati na usisome hati yoyote.
6. Furahia, jivunie na bora zaidi kuwa mhalisi.

Hati/maelekezo au skripti

Video inafaa kuanza kwa wewe kutoa ujumbe mfupi mwepesi kuhusu kile unachofanya ili kuunda wakati bora ujao au kile ambacho ungependa kuona kama wakati bora ujao au siku za usoni. Hii isiwe zaidi ya sentensi moja.

Kisha tamatisha kwa kusema “I am Girl Rising.” Unaposema “I am Girl Rising” unaweza kuonyesha mkono mmoja au mikono yote iliyoandikwa “Girl Rising.”

Tafadhali angalia baadhi ya mifano ya video hapa pamoja na mifano ya hati/ skripti.

“Mimi ni mshauri wa wasichana katika STEM. I am Girl Rising.”

“Mimi ni mtetezi wa usawa wa jinsia. I am Girl Rising.”

“Ningependa kuona maeneo salama kwa wasichana kusoma na kukua. I am Girl Rising.”

“Nafanya kazi kuhusiana na haki ya hali ya hewa. I am Girl Rising.”

“Mimi ni mshirika wa usawa wa jinsia. I am Girl Rising.”

“Ninapigana dhiki ya ndoa za watoto. I am Girl Rising.”

“Ninakuza ufahamu wa afya ya kiakili kwa wasichana wadogo. I am Girl Rising.”

“Ninawapa/ninaunda nafasi katika michezo kwa wasichana. I am Girl Rising.”

“Ninasimama dhidi ya dhulma za kijinsia. I am Girl Rising.”

Lugha.

Tafadhali jisikie huru kuzungumza katika lugha yako ya mama ila sema neno “Girl Rising” katika Kiingereza.

Uwasilishaji

Video yako ikiwa tayari, tafadhali iweke [hapa](#). Kwa kushiriki, unasaidia katika kueneza sauti ya wale ambao wamejitolea kuandaa mustakabali wenye mabadiliko. Asanteni sana kwa kuwa mojawapo wa washiriki wa kamjeni ya “I Am Girl Rising” na kujitolea kwa mustakabali bora! Iwapo una maswali tafadhali jihisi huru kutuma barua pepe kwa Virginia Terry kwenye virginia@girlrising.org.